# WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

## SHULE YA SEKONDARI KINJUMBI

**Kumb.Na. KINJ SS/2019/01** Tarehe………………

MZAZI/ MLEZI WA,

……………………………………………

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KINJUMBI KIDATO MWAKA 2020

**1.0 UTANGULIZI**

Ndg. Mzazi/ mlezi ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari ya Kutwa ya Kinjumbi kidato cha kwana 2020 ili kuendelea na masomo yake. Shule hii ipo kijiji cha Kinjumbi –Kaskazini mwa mji wa Kilwa Masoko takribani 8KM kutoka Somanga.

Ukumbuke kuwa mwanao amebahatika sana kupata nafasi hii muhimu ambayo amepewa na taifa. Mwanao anatakiwa aweke juhudi kubwa sana katika masomo, kazi, michezo pamoja na mwenendo bora wa tabia kwa manufaa yake na taifa kwa ujumla. Aidha mwanao anapaswa kufuata sheria, taratibu na kanuni za shule ili aweze kufikia malengo yake na malengo ya taifa kwa ujumla.

Mwanao anatakiwa atumie vizuri nafasi yake aliyopewa na serikali kwa kusoma masomo yanayotakiwa kusomwa kwa lazima, ambayo ni masomo tisa kama yafuatayo;-

1. CIVICS
2. HISTORY
3. GEOGRAPHY
4. KISWAHILI
5. ENGLISH
6. PHYSICS
7. BIOLOGY
8. CHEMISTRY
9. BASIC MATHEMATICS

Siku ya kuripoti ni tarehe **06/01/2020** unatakiwa kufika shuleni siku hiyo bila ya kukosa kwa ajili ya kuanza masomo**, unatakiwa kuripoti ndani ya siku saba (7) kuanzia tarehe tajwa, ni lazima mwanafunzi afike kuripoti na mzazi au mlezi anayemtegemea ili aweze kutambulika na shule**

## 2.0 MAMBO YA KUZINGATIA

Mzazi / mlezi unatakiwa kuzingatia maagizo yafuatayo ili mwanao aweze kujiunga na shule hii,

### 2.1 SARE ZA SHULE (SCHOOL UNIFORM)

Mwanao anatakiwa kuwa na sare sahhii inayokubalika na uongozi wa shule, mara nyingi wanafunzi wanaleta sare isiyo sahihi (inayobana/ modo) kwa wavulana au sketi fupi kwa wasichamna, mwanao akileta sare ya aina hiyo

**HAITOKUBALIWA NA HAITOPOKELEWA.**

## A. WAVULANA.

- ❖ Suruali mbili za mchono wa linda - jeans staili, suruali za modo hazitakubaliwa
- ❖ Mashati meupe mawili ya mikono mifupi-Yasiyobana.
- ❖ Viatu vyeusi jozi mbili
- ❖ Mkanda mweusi wa ngozi mmoja
- ❖ Soksi nyeusi jozi mbili

## B. WASICHANA

- ❖ Sketi mbili Linda box na zisiwe fupi zifike kwenye kifundo cha mguu.
- ❖ Mashati/blauzi mbili nyeupe za mikono mirefu
- ❖ Viatu vyeusi jozi mbili
- ❖ Soksi ndefu nyeupe jozi mbili
- ❖ Wanafunzi wa kike wanaruhusiwa kuvaa hijabu nyeupe ya kawaida isiyo na mapambo/ marembo – hijabu hiyo iwe ya duara pia iwe ndefu.

**NB;-**

- ➢ Suruali iwe na pindo na tanapu pia iwe pana saizi ya vipimo 20 –chini
- ➢ Viatau visiwe vya kupanda (ngazi), mabuti wala bajaji (kwa wasichana)
- ➢ Hairuhusiwi kuvaa kofia, kandambili, mapambo/urembo wa aina yoyote ile kama vile heleni, bangili, kufu, pete, vikuku, kunyoa kipara, kunyoa kiduku, kusuka, kufuga kucha, rasta nk.

Vitambaa vya sare vinapatikana maeneo karibu na shule SOMANGA kwa wafanya biashara na mafundi cherehani ili kuepusha kununua vitambaa visivyo vya rangi sahihi na visivyo na ubora kwani **HAVITOKUBALIWA**

## C. SARE ZA MICHEZO

### ➢ WASICHANA

- ❖ Fulana moja rangi ya blue (jezi)
- ❖ Raba nyeupe
- ❖ Track suti rangi ya blue

### ➢ WAVULANA

- ❖ Fulana moja rangi ya blue (jezi)
- ❖ Raba za michezo
- ❖ Bukta moja rangi ya blue (jezi)

## D. SARE MAALUMU

- Fulana za shule rangi ya Dhambarau – zinapatikana shuleni kwa Mwanafunzi anunuliwe mara tu afikapo kuripoti shuleni kwa kuwa ni sehem ya sare ya shule.
- Sketi rangi ya Light green (wasichana)
- Suruali rangi dam ya mzee (wavuala)

## E. MAHITAJI KWA AJILI YA USAFI WA MAZINGIRA.

- Aje na panga moja lililonolewa kwa wavulana tu
- Aje na jembe lililonolewa na kuwekwa mpini kwa wasichana tu.

## F. MAHITAJI KWA AJILI YA MASOMO

- Aje na daftari tisa (9)
- Aje na kalamu na mkebe wa hesabu
- Aje na begi ya kubebea madaftari na vifaa vyake vingine ya masomo.

## G. AFYA

Kabla ya kufika shuleni hakikisha kuwa mwanao umempima afya yake vizuri kwa mganga wa serikali na kujaza kikamilifu fomu iliyoambatanishwa.

# 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa ka mujibu wa sheria na kanuni za Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha shule hii inazingatia miongozo yote ya Elimu inauotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Technolojiayenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye jukumu na usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

Mwanao anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa kirefu kwa maandishi mara baada ya kuripoti hapa sjuleni. Mambo hayo ni pamojao na ;-

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla.
- Mahudhurio mazuri katiaka kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni Lazima
- Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya kujisomea jioni ( preparation)
- Kuwahi katika kila shughuli ya za shule na nyingine utakazopewa.

- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani ya nje ya mipaka hiyo kwa muda wako waote katiaka shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule kwa ujumla.
- Kuvaa sare ya shule muda wate unapotakiwa kufanya hivyo huwapo ndani na nje ya mipaka ya shule.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- Kutunza mali za shule na umma kea ujumla .

### 3.1 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- Wizi
- Ubakaji
- Ulevi na matumizi mengine ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, ugolo nk.
- Kupigana au kupiga
- Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
- Kudharau bendera ya Taifa
- Kudharau wimbo wa Taifa
- Kupata au kusababisha mimba
- Kutoa mimba
- Kuoa au kuolewa
- Kukataa adhabu kwa makusudi
- Kugoma, kuchochea au kushiriki kuvuruga amani ya shule na usalama wa shule kwa ujumla.
- Kuwa na simu ya mkononi

### 3.2 . MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

- ✓ Fomu ya afya iliyojazwa na mganga wa serikaki
- ✓ Cheti cha kuzaliwa au kumbukumbu sahii ya tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi
- ✓ Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na Sheria, kanuni na taratibu za shule

NB;**- Tafadhari soma kwa makini maelezo haya na kuyaelewa kikamilifu.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……………………………….

**EZEKIEL MULULA**

**MKUU WA SHULE**